JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI - TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE.

SHULE YA SEKONDARI MANG'OTO, S. L. P. 134, MAKETE.

SIMU 0757 297 383/ 0623 632 0/470625 842 741

TAREHE 04/12/2020

Kumb.Na. MASS/JI/VOL.4 /2020/15

Jina la mwanafunzi.....
Jina la shule ya msingi.....
Anuani.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI **MANG'OTO**, WILAYA YA MAKETE MKOA WA **NJOMBE** MWAKA 2021.

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari ya Mang'oto ipo umbali wa km 56 kutoka Makete Mjini. Ipo mkoa wa Njombe katika Halmashauri ya Makete. Usafiri wa basi kutoka mjini Makete unapatikana. Nauli ni Tshs 5,000/= kutoka Makate Mjini na pia ni hiyohiyo kutoka Njombe Mjini. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia.

2.1 Sare za Shule

i. WASICHANA: Suruali mbili moja ni rangi ya damu ya mzee na ya pili ni nyeusi sambamba na sketi fupi zinazopita kidogo magotini zenye marinda.
WAVULANA: Suruali mbili moja ni rangi ya damu ya mzee na ya pili ni nyeusi.
ii. Uje na mashati mawili kwa wavulana na blauzi mbili kwa wasichana wote ni mikono mirefu.
iii. Uje na hijabu ya rangi nyeupe. Hii ni kwa waislamu tu.
iv. Uje na sare za michezo Truck suit nyeusi zenye ufito mweupe kwa wote. Pia uje na raba /viatu na bukta kwa wavulana na sketi kwa wasichana kwa ajili ya michezo.
v. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba jozi mbili visivyo na kisigino kirefu kwa wavulana na wasichana.
vi. Soksi za rangi nyeusi kwa wavulana jozi mbili, na soksi nyeupe kwa wasichana nao jozi mbili au zaidi.
vii. Sweta rangi za damu ya mzee (zenye mshono wa V shingoni) kwa wavulana na wasichana.
viii. Pia uje na tai nyeusi na damu ya mzee na kwa wasichana scaff nyeusi na damu ya mzee (scaff ziwe na ufito mweupe pembeni na ziwe ndefu kutosha (pia zinapatikana shuleni).

2.2 Daftari (Counterbooks 10), kalamu, rula na mkebe wenye vifaa vya hesabu, pamoja na begi la kuchukulia vifaa vya darasani.

2.3 Rimu moja (Karatasi za A4 NYEUPE) kwa ajili ya majaribio ya ndani (Huduma ya duka la shule ipo)

2.4 Aje na pullneck nyeusi na kofia ya rangi ya bendera ya Taifa.

2.5 Chakula cha wanafunzi wa hosteli:
Utaratibu wa chakula shuleni unasimamiwa na wazazi na fedha za chakula hulipwa kupitia: Jina la Akaunti: WAZAZI MANG'OTO. Akaunti ni NMB Namba: 60410010400. Kiasi cha mchango hubadilikabadilika kutokana na kamati ya chakula inavyopanga kwa kila robo muhula. Na hiyo hutegemea idadi ya siku watoto wanazokaa shuleni, na bei za vyakula za wakati huo. Kwa robo hii watachangia 71,500/= kwa mwaka ni 286,000/=

2.6 Mahitaji mengine muhimu ni tranka kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake, Godoro la nchi 2.5, blanketi zito moja, mashuka mawili PINKI na BLUU BAHARI, mto wenye folonya, taulo, ndoo 2 moja ya kuogea na moja ya usafi wa mazingira, bakuli (Kontena), kijiko, kikombe, kigaloni kidogo kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa, dawa ya mswaki na mswaki, kiwi ya viatu, ndala, Wasichana pia waje na kanga/kitenge kimoja na pedi za kutosha.

2.7 Vifaa vya usafi, mfagio(brumu)/, jembe 1 (lenye mpini), na slesha (wavulana) na panga (wasichana). Viwe vipya.

2.8 Kwa kuwa shule ni ya Hostlei inayosimamiwa na wazazi unatakiwa kufika na Tshs 10,000.00 kwa ajili ya ukarabati wa bweni.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

SHERIA ZA SHULE

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation).
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kazingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kutunza heshima na jina la shule pamoja na kuifanya shule mahali pa amani.
(i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, na
(j) Kutunza mali za umma.

3.2 **Makosa yafuatayo yanawezakusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule**

a) Wizi
b) Uasherati, ushoga na Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba au kusababisha mimba.
h) Kuoa au kuolewa
i) Kutoa mimba
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kuwa na simu ya mkononi.

4.0 **Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical Examination form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali au Ikonda Hospitali, baada ya kupimwa. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. Imeambatanishwa.
b) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. (Imeambatanishwa).

NB: Serikali inatoa huduma ya kwanza shuleni na mtoto akizidiwa mzazi utagharimia matibabu nje ya shule. Jitahidi mwanao awe na BIMA YA AFYA na afike nayo shuleni.

4.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

5.0 Mwanao aje na mafaili mawili moja kwa ajili yake na jingine la kuwekea kumbukumbu zake za kitaaluma. Pia aje na DICTIONERY - ENGLISH TO ENGLISH

NB: Mwanao afike shuleni tarehe **11/01/2021**

Pia mzazi au mlezi uje na namba yako ya simu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA MANG'OTO

.....

BONAVENTURA PANGANI MGAYA

MKUU WA SHULE.

FOMU YA MZAZI NA MWANAFUNZI KUKUBALIANA NA KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Sehemu ya mzazi/ mlezi

Kwa Mzazi/ Mlezi wa.....

1. Napenda kukupongeza kwa mwanao kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza hapa Mang'oto. Ni mategemeo ya shule kuwa utajitahidi kwa uwezo wako wote kumsaidia ili aweze kusoma bila matatizo (kwa kumtimizia mahitaji yote ya muhimu kwa wakati). Mzazi anaruhusiwa kuleta mahitaji ya mtoto kila jumamosi ya kwanza ya mwezi saa 04:00 hadi saa kumi.
2. Ili mtoto wako aweze kufanikiwa ni muhimu awepo shuleni muda wote wa masomo. Hivyo huna budi kumsaidia ili vikwazo visivyo vya lazima visiwepo.
3. Tafadhali jaza fomu iliyoambatanishwa kama inavyojieleza.
4. Msaidie mwanao awe na BIMA YA AFYA na aje nayo shuleni itatunzwa na mkuu wa shule.
5. Ni kosa kubwa kutompeleka mwanao shuleni. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kukaidi agizo hili la kiserikali.

A: AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi.....

Mzazi/Mlezi wa (jina la mtoto).....

ninakubali aingie shule ya sekondari Mang'oto na ninaahidi kumtimizia mahitaji yote yaliyoagizwa.

Pia naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule kumlea na kumtunza ki- Tanzania (awapo shuleni na likizo) mpaka atakapo maliza masomo yake. Na kama kuna mabadiliko nitautaarifu uongozi wa shule.

Anuani yangu ya kudumu:.....SIMU .....

Sahihi.....Tarehe.....

B: AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi..... Nakubali Nafasi niliyopewa katika shule ya Sekondari ya Mang'oto. Naahidi kuwa nitazitii sheria zote za shule na kufuata maelezo na maagizo nitakayopewa na Mkuu wa Shule, Wafanyakazi wote na viongozi wote wa Serikali ya wanafunzi. Nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, Elimu ya kujitegemea, Michezo na kutunza usafi wa mazingira ya shule kwa muda wote nitakao kuwa Mang'oto.

Shule niliyosoma ni.....Namba ya mtihani ni.....

Sahihi.....Tarehe.....

NB: Maelezo haya yajazwe kabla ya kufika shuleni.

. SEHEMU YA MGANGA.

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING
MANG'OTO SECONDARY SCHOOL
(REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION)

This form must be completed by a Government Medical Officer.

Name of student.....

Age..... Sex .....
The above named student has been examined in respect of

a) PREGNANT TEST (FOR GIRLS ONLY).....
b) STOOL.....
c) URINE.....
d) CHEST .....
e) BLOOD .....
f) EYES .....
g) EARS.....
h) HAEMAGLOBIN .....
i) P.V. BLEEDING .....
j) ASTHMA .....
k) SKIN DESEASE .....
l) LEPROSY .....
m) EPILEPSY .....
n) ANY DEFORMITY .....
o) T.B .....
p) NEUROSIS .....
q) VENEREAL DISEASE .....
r) OTHER FINDINGS.....
……
……

I am satisfied that the above student is fit/not fit for pursuing Secondary studies at MANG'OTO SECONDARY SCHOOL.

....
SIGNATURE DATE.

....
DESIGNATION and OFFICIAL STAMP STATION